MWONGOZO WA UPIMAJI PLOTI ZA KUDUMU SEOSAW

Ukinukuu mwongozo huu, tafadhali taja kama:

SEOSAW partnership (2021). A network to understand the changing socio-ecology of the southern African woodlands (SEOSAW): Challenges, benefits, and methods. *Plants, People, Planet*, *3*(3), 249-267. doi: 10.1002/ppp3.10168.

Casey M. Ryan, Nicholas Berry, Stephen Syampungani, Francisco Maiato Gonçalves, Steve Makungwa, Benjamin Wigley, Manfred Finckh, Nicola Stevens, Caroline Lehmann, Mat Williams, Mylor iNgoy Shutcha , Jonathan Ilunga Muledi, Sally Archibald, Wayne Twine, Isla Grundy, Carla Staver, Anderson Muchawona, Benard Guedes, Adeline Fayolle, Josiah Katani, Nicholas Berry, Edward Mitchard, Kyle Dexter, Iain McNicol, Rose Pritchard, Emily Woollen, Thom Brade, Ellie Wood, Sam Bowers, John L. Godlee, Geoff Wells, David Bauman , Oliver Phillips, Penny Mograbi, Lorena Benitez.

Imetafsiriwa (English - Swahili) na Elisha Elifuraha Njoghomi

Shukrani

Utayarishaji wa mwongozo huu wa upimaji wa ploti za kudumu umewezeshwa na mradi wa SEOSAW unaofadhiliwa na NERC. Kwa shemu kubwa, mwongozo unatokana na mwongozo wa RAINFOR (Phillips, Baker, Feldpausch, & Brienen, 2016). Mabaki ya miti iliyokufa na kukauka kulingana na (Waddell, 2002) na itifaki za upimaji wa Visiki zilitengenezwa kama sehemu na mradi wa ACES unaofadhiliwa na ESPA (DFID/ESRC/NERC). Kazi hii pia iliungwa mkono na Mfuko wa Kuongeza Kasi ya Matokeo wa GCRF. Tafsiri ilifadhiliwa na Mradi wa SECO unaofadhiliwa na NERC.

V3.6

Yaliyomo

1.0 UTANGULIZI 3
2.0 MUHTASARI 4
2.1 Muundo wa ploti 4
2.2 Mashina ya miti 4
3.0 USIMIKAJI WA PLOTI 7
3.1 Kushirikiana na watumiaji na wamiliki wa ardhi 7
3.2 Eneo la kusimika ploti 7
..... 8
3.3 Maumbo na mwelekeo wa ploti 8
3.3.1 Kukadiria mteremko 9
3.4 Eneo la ploti 9
3.5 Msimu wa uwekaji na upimaji wa ploti 9
3.6 Upatikanaji na mwonekano wa ploti 9
3.7 Jinsi ya kuunganisha mzunguko wa ploti 10
3.8 Kurekodi data 10
4. MASHINA YA MITI 11
4.1 Nini cha kupima 11
4.2 Kipimo cha kipenyo 12
4.2.1 Sehemu ya Kupimia Kipenyo 12
4.2.2 Kupima kipenyo 13
4.3 Kuweka alama na kuchora mashina 14
4.3.1 Kuashiria mashina 14
4.3.2 Uramanishaji wa mashina ya miti 15
4.3.3 Mashina yaliyokatwa, yaliyovunjika na kuanguka 16
4.4 Sifa nyingine za mashina hai 16
4.5 Uharibifu na vifo kwenye mashina ya miti 16
4.5.1 Mashina yanazochipuka 17
4.6 Utambuzi wa aina miti 17
4.7 Kupima urefu wa mti 19
5.0 VISIKI 20
6.0 SENSA YA MARUDIO YA MITI YOTE 20
6.1 Upimaji wa miti 23
6.2 Miti Nyongeza mzingo mipya 23
6.3 Miti iliyopotea 23

7.0 PLOTI ZILIZOHARIBIKA KABISA AU ZILIZOATHIRIWA VINGINENYO 24
7.1 Kwa nini upimaji wa ploti vilivyoathiriwa ni wa thamani 24
7.2 Jinsi ya kufanya uchunguzi kwenye ploti iyoathirika 24
7.2.1 Jinsi ya kukusanya takwimu za ngazi ya shina 26
8.0 KIAMBATISHO 1: MUUNDO WA FOMU YA DATA ZA PLOTI 27
9.0 Kiambatisho 2: Fomu ya kujaza data za miti 35
10.0 KIAMBATISHO 3: Kutumia ndege isiyo na rubani kutafuta viwanja vipya.................................. 38
Thom Brade 38
10.1 Uendeshaji wa Droni - iOS au kifaa cha Androidi 38
10.2 Uchakataji wa data za droni 38
11.0 KIAMBATISHO 4: Kuweka tagi miti nyongeza mzigo wakati wa upimaji wa kiwanja 39
12.0 BIBLIOGRAFI 40

1.0 UTANGULIZI

Mwongozo huu wa upimaji wa misitu unaelezea mbinu za kuanzisha ploti za kudumu kwa ajili ya tafiti mbalimbali kwa maeneo ya misitu ya savana, miombo, na misitu ya ukanda mkame .Inazingatia uanzishwaji wa ploti za kudumu lakini pia ni muhimu kwa zile ploti za muda mfupi. Kufuatana na mwongozo huu, na kutumia data zinashoshabihiana, kutahakikisha utangamano na watafiti wengine wanaofanya kazi kusini mwa Afrika, na hii itaruhusu kuunganishwa kikamilifu katika kupata ulinganifu wa kimataifa pia. Lengo kuu ni kubadilishana uzoefu kuhusu kile kinachofanya kazi na kisichofanya kazi, ili kuepuka kurudiwa kwa makosa katika mbinu hizi za ukusanyaji wa takwimu. Kwa ujumla, kutakuwa na mbinu mbalimbali za uchukuaji wa sampuli zenye kiwango kikubwa cha ufanisi na wingi wa taarifa iwezekanavyo, ambazo zinaweza kutumika katika maeneo tofauti tofauti. Hata hivyo, katika hali tofauti tofauti, mbinu hizi zinaweza kushindwa kufanya kazi sawasawa katika maeneo mbalimbali ya nyika, misitu ya milimani na ile ya ukanda mkame iliyopo Kusini mwa Afrika, pia kuwa na mwingiliano mdogo wa viwango vya kimataifa vinavyoibuka. Njia zilizopendekezwa hapa ni maelewano mazuri, ambayo yanapaswa kumwacha kila mtu (angalau kwa kiwangi kidogo) bila furaha.

2.0 MUHTASARI

2.1 Muundo wa ploti

a. Weka ploti kwenye maeneo yenye uwiano sawa, kulingana na aina ya udongo na historia ya matumizi ya ardhi.
b. Pata ridhaa ya wamiliki wa ardhi na watumiaji wa ardhi wasio rasmi kabla ya kuanza kuweka ploti.
c. Kwa ajili ya ufuatiliaji wa muda mrefu, inapendekezwa kuanzisha ploti zenye ukubwa wa hekta 0.25, 0.5 au 1.0; ploti za miraba zenye eneo la hekta 1.0 zinafaa zaidi kwa muktadha huu.
d. Pima kipenyo usawa wa kifua (DBH) kwa miti yote juu ya kizingiti cha kipenyo k.m. kipenyo cha sm > 5 au sm10. Urefu wa kipenyo katika usawa wa kifua ni mita 1.3 (Kipenyo au mita 0.3 (kwa visiki vilivyokatwa).
e. Weka alama inayoonekana kwenye pembe za ploti za kudumu (au katikati, kwa zile ploti za mduara) kwa kutumia saruji au chuma.
f. Rudia kupima upya miti yote takriban kila baada ya miaka 3. Ziara za kuetmbelea ploti mara kwa mara zaidi mwanzoni zinashauriwa.
g. Kamilisha ujazaji wa fomu za data zinazohitajika kwa kila ploti. Mfano, fomu za data na lahajedwali za kuingiza data zinapatikana kwenye tovuti ya SEOSAW. Pia tazama sehemu ya 8 na 9 kwa uchanganuzi wa nyanja hizi.

2.2 Mashina ya miti

Jedwali la 1: Sifa za kila shina zinazopaswa kurekodiwa (NB: shina, si mti - pima mashina yote, yaliyo hai au yaliyokufa, yaliyosimama au yaliyoanguka). Haya yanachukuliwa kuwa ya kiwango cha chini zaidi kinachohitajika kujibu maswali mengi muhimu ya ushirikiano wa SEOSAW. Wengine wengi bila shaka wanaweza kuongezwa. Mfano laha za data na lahajedwali za kuingiza data zinapatikana kwenye tovuti ya SEOSAW. Pia tazama sehemu ya 9 kwa uchanganuzi kamili wa mashamba ya shina.

Sifa	**Malengo**	**Mapendekezo**
Namba ya utambulisho (ID ya Tagi / au Number ya shina (kama haina tagi)	Kutofautisha mashina ya miti	Weka tagi mashina yote yanayokidhi vigezo. Pigilia msumari kibati cha tagi sm 20 juu eneo wa eneo la kupimia kipenyo (POM)

Kipenyo cha mti	Ukadiriaji wa biomasi ya mti; kiwango cha ukuaji	Eneo la Kupimia kipenyo cha Mti (POM) linafaa kuwa urefu wa mita 1.3 au 0.3 kutoka usawa wa ardhi kwenye mstari mnyoofu (SIO Kwa wima). Upimaji kwa kutumia Kamba ya kupimia unapendekezwa zaidi. Hakikisha kuwa eneo la kupimia kipenyo (POM) linawakilisha kwa usahihi shina la mti husika. Pima sehemu ya juu ikiwa POM ina makovu, matawi n.k. Rekodi urefu wa POM endapo inapaswa kusogezwa juu au chini ya urefu unaopendekezwa.
Sehemu ya kipimia Kipenyo cha Miti (POM)	Kama hapo juu	Hakikisha umerekodi urefu sahihi ulikopimia kipenyo (POM)
Miti yenye mashina zaidi ya moja	Ukadiriaji wa baomasi ya mti, mfumo uotapya na uchipuaji	Rekodi numba ya mti (ID)/ namba ya tagi ya mashina mengine yanaochiphkia kwenye shina kuu.cPima mashina yote yanayokidhi vigezo, hata kama yanatokea shina moja.
Aina za miti	Kuangalia utofauti wa miti kwa koo na jamii, pia inahitajika kwa ajili ya ukadiriaji wa wiani ya biomasi ya mti	Ambatana na mtaalam wa utambuzi wa mimea kama inawezekana, au chukua sampuli kama inawezekana tumia majina ya kienyeji na maumbile ya majani kutambua aina za miti.
Mti hai/ mfu na chanzo cha kifo/kukauka	Kujifunza kuusu vifo vya miti kiwango cha uchipuaji	Pima miti yote hata kama imekufa. Angalia kipengele cha 4.5 kujua vifupisho vya kutumia unaporekodi uharibifu na vifo vya miti
Miti iliyosimama/iliyoanguka	Kujua kama mti umeanguka ni muhimu kwa ajili ya kuelezea kutokuwepo kwake na sababu yake.	Jumuisha miti yote iliyoanguka/iliyolala maadam bado imejishikiza ardhini na ina sehem ya kupimia kipenyo
Miti iliyovunjika	Ukadiriaji wa biomasi ya mti	Rekodi urefu wa mti mahali ulipovunjikia
Uharibifu	Ukadiriaji wa vifo na ukuaji	Kadiria eneo la gamba lililo wazi bila kusahau kama kuna uwepo wa kuvu
Sifa nyinginezo	Angalia kipengele cha 4.4	Haya ni makadirio mepesi na huongeza mfanano la wa takwimu kwenye viwango wa kimataifa.

Mahali shina lilipojikita (changuo lako)	Ni muhimu kwa ufuatiliaji wa tagi zinapopotea ama kwa ajili ya uchambuzi wa majira ya nukta	Rekodi umbali kwa mita kutoka kona ya kusini-magharibi mwa ploti (jira mlalo,x na jirawima,y). Kwa ploti kubwa,gawanya ploti kwenye safu za mita 10. Kwa ploti za duara, rekodi ukingo wa ploti na umbali toka kitovu cha ploti.
Mabaki ya miti iliyokufa (changuo lako)	Kwa uboreshaji wa makadirio ya biomasi na sifa za fomyula mbalimbali	Kama kuna uhusiano imara kati ya Kipenyo kwenye usawa wa kifua (DBH) na urefu wa mti, basi, pima urefu wa miti kwa seti ya miti 100 kwa kila eneo.Kama kuna uhusiano dhaifu kati ya Dbh na urefu, pima urefu wa miti yote. Angalia kipengele cha 4.7 kwenye mbinu za upimaji.
Miti nyongeza mzigo	Inahitajika kwa ajili ya kuangalia hewa ukaa, na kuchambua mienendo ya sensa ya miti	Kwa ploti zilizopo tayari, andikisha machipukizi yote yanayokizi vigezo na masharti katika karatasi tofauti.
Visiki	Ukokotoaji wa ”biomasi iliyopotea kupitia ukataji miti” na pale inapowezekezana ionyeshe vyazo vya upotevu	Pima kipenyo kwa kila kisiki chenye unene wa zaidi ya sm 5 (>sm 5). Rekodi pia urefu wa kisiki husika kilipopimiwa kipenyo chake. Angalia kipengele cha 7
Miti midogo (Changuo lako)	Angalia itifaki yake kwenye tovuti SEOSAW website	
Mabaki ya miti (chaguo lako)	Angalia itifaki yake kwenye tovuti SEOSAW website	
Udongo (changuo lako)	Angalia itifaki yake kwenye tovuti SEOSAW website	
Nyasi, jamii za mibuabua, miche (changuo lako)	Angalia itifaki yake kwenye tovuti SEOSAW website	

3.0 USIMIKAJI WA PLOTI

3.1 Kushirikiana na watumiaji na wamiliki wa ardhi

Hakikisha unashirikiana na wenyeji, watumiaji na wamiliki wa ardhi wote. Ni vema kuwa mwangalifu kwa sababu hawa wanaweza kuwa vikundi tofauti. k.m. ardhi inaweza kuwa ya kibinafsi au ya serikali, lakini wenyeji wanaweza kuvuna kuni au mazao mengine yasiyo mbao. Kiwango cha chini cha ushirikishwaji chaweza kuhusisha mkutano wa wanajamii husika kabla na baada ya kumaliza kazi ya kuweka ploti. Kushirikisha wanajamii katika kazi ya uwekaji wa ploti kunaweza kuwa na manufaa kwa wote na ni njia nzuri ya kuhakikisha kwamba jumuiya ya eneo hilo inafahamishwa kikamilifu kuhusu eneo ziliko ploti na kile kinachofanyika kwenye ploti hizo. Hii inaweza kupunguza uwezekano wa kutokea migogoro kuhusu madhumuni na asili ya kazi. Toa taarifa kwa njia ya maandishi kwa watumiaji wa ardhi na wenyeji kutumia lugha rahisi inayoeleweka ili iweze kuwafikia walengwa wote katika jamii. Kama inawezekana, pata idhini ya kimaadili katika taasisi yako kwa ajili ya kazi hiyo.

Inashauriwa kuwaajulisha watumiaji na wamiliki wa ardhi kuhusu matokeo muhimu ya utafiti, haswa kutokea kwenye ploti za kudumu ambapo wadau wanashirikishwa mara kwa mara. Hii inaweza kufanyika kwa mfumo wa usambazaji wa angalau, ripoti ndogo ndogo zilizofasiriwa. Hata hivyo, mikutano ya kijamii ya ana kwa ana inayowezesha mazungumzo kati ya watafiti na washikadau wengine ina manufaa kwa pande zote, ikiruhusu ujumuishaji wa maarifa asilia na majadiliano kuhusu vipaumbele vya utafiti vya washikadau, pamoja na malengo na mipango zaidi ya watafiti.

3.2 Eneo la kusimika ploti

Ploti mpya zinapaswa kusimikwa ndani ya maeneo ambayo yanakidhi vigezo vifuatavyo:

a. Eneo lenye uwiano sawa wa udongo na chembe chembe asilia za miamba
b. Eneo lenye uwiano sawa wa matumizi ya ardhi na historia ya matumizi ya ardhi
c. Ridhaa iliyotolewa na wamiliki wa ardhi na watumiaji wa ardhi wazawa kwa ajili ya usimikwaji wa ploti za ridhaa ya kutembelewa na watafiti inapohitajika.
d. Uwezekano wa kuifikia ploti - ingawa ploti zilizoko karibu na barabara, njia na makazi zina uwezekano mkubwa wa kuathiriwa na mwingiliano wa shughuliza binadam, kwa hivyo ni lazima kwa makini katika kusimika ploti na kuchukua sampuli maeneo kama haya, kwa mfano kwa kutafuta angalau kilomita 1 kutoka kwa vipengele tajwa hapo juu.
e. Msaada wa kitaasisi wa muda mrefu – Ni muhimu kuwa na uhakika wa usimamizi endelevu wa ploti toka kwenye taasisi husika.
f. Uwezekano wa kutokubadilishwa kabisa kwa matumizi ya ardhi hiyo; - ingawa ploti mpya hazipaswi kuwekwa mahususi katika maeneo ambayo hayana usumbufu wa kibinadamu kwani usumbufu kama huo unapatikana kila mahali na unahitaji kueleweka. Kwa hivyo ni muhimu kujumuisha ploti zinazotumika kwa kilimo cha kuhama-hama, au kuvunwa kwa mbao, mkaa au nguzo za kujengea.

Wakati fulani, uwekaji wa ploti unaweza kuwa na hali ya upendeleo hasa kwenye maeneo ambayo yanaonekana kuwa rahisi kufanya kazi au maeneo ambayo yanatimiza vigezo vya awali. Ili kuepuka uwezekano wa kuwa na upendeleo katika maeneo hayo, inashauriwa ploti

mpya kuwekwa bila mpangilio, au kwa mpangilio uliobainishwa awali, ndani ya matabaka ambayo yanakidhi vigezo vilivyo hapo juu. Ploti zilivyopangwa mara kwa mara (k.m. kwenye gridi ya taifa) zina manufaa hasa wakati wa uchambuzi wa takwimu.

Kuamua maeneo ya kamba za kupimia kipenyo nasibu

Ili kupata kamba za kupimia kipenyo zisizo na mpangilio, kabla ya kwenda prini unweza tumia kifaa cha GIS kuweka alama kwa nasibu ndani ya matabaka ya kupendeza na kupakia pointi hizi kwenye GPS. Weka angalau mara mbili ya idadi ya pointi, na utumie pointi zisizo za kawaida pekee, ukihifadhi pointi zilizohesabiwa kama hifadhi ikiwa nambari isiyo ya kawaida haifikii vigezo vilivyo hapo juu.

Kompyuta zenye uwezo wa kufikia taswira ya satelaiti na ubora wa juu inaweza kusaidia kubainisha kama maeneo yanayoweza kutokea ya kamba za kupimia kipenyo yanakidhi vigezo vilivyo hapo juu k.m. kwa kutambua tofauti kutokana na aina ya udongo na vipengele vya kihaidrolojia, na ishara za matumizi ya binadamu. Programu zinazofaa zinazopatikana mwaka wa 2018 ni pamoja na MotionXPro (iOS) au Gaia GPS (Android na iOS).

Kutumia Droni katika kuainisha eneo la kamba za kupimia kipenyo

Kutumia ndege isiyo na rubani (droni) kunaweza kuwa na manufaa makubwa katika kutathmini uwezekano wa eneo linalofaa kwa usimikaji wa kamba za kupimia kipenyo kulingana na ukaribu na mwingiliano wa shughuliza binadamu, vijito vya msimu n.k ambayo inaweza kuhitaji juhudi kubwa kugundua au kusababisha maeneo yasiyofaa kwa usimikaji wa kamba za kupimia kipenyo za muda mrefu. Tazama sehemu ya 10.

3.3 Maumbo na mwelekeo wa ploti

Maamuzi juu ya umbo la ploti hutegemea zaidi uhitaji wa eneo litakalotosheleza usimikwaji wa ploti ndani ya tabaka moja la uoto lenye uwiano sahihi wa mzingo:eneo - ambao huathiri idadi ya miti kwenye kingo za ploti, na urahisi wa uwekaji wa ploti.

Kwa kawaida, mtandao wa SEOSAW unajumuisha ploti za mviringo, mraba na mstatili. Miduara ina uwiano mdogo zaidi wa mzingo:eneo na ni rahisi katika uwekaji wake, haswa katika maeneo wazi, lakini inaweza kuwa ngumu kupima ikiwa itazidi nusu-kipenyo cha mita 20. Kwa ploti kubwa, miraba au mistatili ni rahisi kuweka na inapendekezwa kwa ploti mpya zenye eneo la hekta 0.2 au zaidi. Inapowezekana, ploti za mraba zinapendekezwa kwa kuwa zina uwiano mdogo wa mzingo: eneo kuliko mistatili, ingawa ploti za mstatili zinaweza kusaidia upatikanaji wa eneo la kutosha kuweka ploti zote ndani ya tabaka moja.

Inapowezekana, ncha kuu za ploti zielekezwe upande wa Kaskazini/Kusini na Mashariki/Magharibi kwa ploti za mraba na mstatili, pamoja na hayo, marekebisho madogo juu ya mwelekeo yanaweza kufanyika ili kuifanya ploti iwe ndani ya eneo moja lenye tabaka moja la uoto na undongo. Inapendekezwa kuwa mwanzo wa mweleko wa ncha kuu za ploti uanzie kona ya Kusini-Magharibi mwa ploti. Vile vile, longitudo, latitudo na mwinuko katika sehemu ya kuanzia lazima virekodiwe.

Maelezo ya mteremko wakati wa kuanzisha kamba za kupimia kipenyo

Kamba za kupimia kipenyo mpya zinapaswa kuanzishwa ili kupata sampuli ya eneo fulani la ardhi, badala ya makadirio tu. Hii inahitaji ufundi na namna ya kukubaliana na jinsi mwelekeo na urefu wa jira-x na jira-y wakati wa kufunga upande wa mwisho wa kamba za kupimia kipenyo za mraba au mstatili. Ili kusahihisha mteremko na kuruhusu ulinganisho na kamba za kupimia kipenyo ambavyo sampuli ya eneo lililopangwa, wastani wa mteremko na kipengele

3.3.1 Kukadiria mteremko

Mteremko unaweza kupimwa kwa kutumia vifaa tofauti tofauti kama vile klinomita na kitafuta masafa kama leza. Mteremko unapaswa kupimwa katika sehemu nyingi ndani ya eneo la ploti na kisha kutafuta wastani wake. Jaribu kupima mteremko juu ya angalau pointi tano zilizoenea juu ya ploti. Pamoja na kujua kiwango cha mteremko, ni vema pia kuripoti mwelekeo wa mteremko katika kiwango cha nyuzi.

3.4 Eneo la ploti

Kiwango sahihi cha eneo la ploti hutegemea malengo ya utafiti na sifa za tabaka inakochukuliwa sampuli. Ploti ndogo ndogo zina uwiano wa juu kati ya mzingo: eneo na kwa kawaida hutoa makadirio ya biomasi ambayo yanaweza kuwa na mtwanyiko hasi au chanya unaoonyesha uepndeleo, na vile vile, mbinu hii sio njia muafaka pale inahusianishwa na matumizi ya teknologia ya satelite kuwa na mgawo mkubwa zaidi wa tofauti kuliko ploti kubwa. Ploti za ukubwa wa hekta moja zimekubaliwa kuwa ni kiwango kinachootumika na watafiti katika nchi zenye msitu ya ukanda wa mvua nyingi na inapendekezwa kwa maeneo ya ufuatiliaji wa muda mrefu katika mtandao wa SEOSAW. Katika maeneo ya wazi, ploti kubwa zinaweza kuhitajika ili kuhakikisha kuna mashina ya miti zaidi ya 200 yalichukuliwa kama sampuli. Sampuli zanye ashina machache kuliko hii inaweza kupelekea ukadiriaji wa vifo vya miti kuwa sio sahihi sana.

Kwa ploti zisizo za kudumu, na ploti zenye ukubwa wa ha 0.75, ha 0.5 na ha 0.25 zinakukubalika pia katika maeneo ya misitu yenye mfanano mkubwa wa aina na saizi za miti. Ploti zenye mashina chini ya 25 ndani yake havifai kwa ukadiriaji wa aina mbalimbali za miti na vinapaswa kuongezwa ukubwa.

3.5 Msimu wa uwekaji na upimaji wa ploti

Tofauti katika uwiano wa kiasi cha maji kwenye mti inaweza kuathiri vipimo vya kipenyo. Kwa hivyo, ikiwa ploti zitapimwa tena, ni vyema vipimo vifanywe kwa wakati mmoja wa mwaka. Vipimo vya miti kwa kawaida huwa rahisi wakati wa kiangazi kunapokuwa na tabaka dogo uoto chini ya msitu. Lakini inaweza pia kuwa muhimu kutembelea ploti wakati wa msimu wa mvua ili kukusanya vocha za mimea midogo ya msimu kwa ajili ya utambuzi hebariumu.Hii pia inawez kuongeza uwezekano wa kupata maua au matunda ambayo huongeza usahihi wa wakati wa utambuzi wa spishi za miti.

3.6 Upatikanaji na mwonekano wa ploti

Kwa ploti za ufuatiliaji wa muda mrefu, alama za kudumu ziwekwe kwenye pembe za ploti za mraba au mstatili ama katikati ya ploti za mviringo. Katika baadhi ya maeneo, kuweka alama kwenye eneo la ploto kunaweza kuathiri jinsi ploti inavyotumiwa na watu, na hivyo kusababisha uwezekano wa kuleta upendeleo kwa sampuli. Katika hali hizi, miti haipaswi kuwekewa alama au kutambulishwa kwa njia inayoonekana (lebo zilizozikwa au ramani za kina za maeneo ya miti zinaweza kutumika badala yake), na eneo la ploti linapaswa kutiwa alama kwa njia za siri. Vitu vinazotumiwa kuashiria maeneo ya ploti hizi lazima viwe vya kudumu kwa muda mrefu wa kutosha ili zitunzwe kati ya matukio ya kipimo na zisiharibiwe na kutu, moto, mchwa, n.k. Kuongeza alama za ziada, k.m. kwenye gridi ya mita 20 ndani ya ploti, na kwa vipande vya mita 10 kuzunguka mpaka, inaweza kusaidia kupunguza makosa ya kujumuisha/kutengwa kwenye upimaji upya, na kutafuta tena mahali miti ambayo inapoteza vitambulisho vyake.

3.7 Jinsi ya kuunganisha mzunguko wa ploti

Mara baada ya kupata sehemu ya kuanzia kwa mzunguko wa mraba au mstatili wa ploti, mipaka ya ploti inapaswa kupimwa kwa uangalifu kwa kutumia dira na kipimo cha ploti, angalau watu wawili watahitajika kwa ajili ya kazi hii: mmoja kushikilia dira na mwingine kupima umbali. Funga kamba kufuata ya mipaka ya ploti. Ukataji wowote wa mimea ndani au karibu na ploti unapaswa kuepukwa kwa kila hali kila inapowezekana. Kuongeza kamba zinazotumia urefu wa ploti kwa umbali wa mita 10 au 20 kunaweza kusaidia katika mwelekeo wakati wa kufanya vipimo na kuchora ramani ya maeneo ya miti (ona sehemu ya 4.3.2).

Mahitaji ya uwekaji wa mipaka ya ploti

- Nguzo za mbao zilizowekwa dawa (kipenyo cha sentimita 15) hudumu kama miaka 10, hata kwa kuchomwa mara kwa mara. Hizi zinahitaji kuchimbiwa vizuri, hata hivyo, hii si kazi rahisi.
- Nguzo za zege zilizo na upau wa kuimarisha ndani (40 x 10 x 10 cm) mara nyingi zinaweza kutengenezwa ndani na ni za kudumu zaidi kuliko mbao. Ikiwa nguzo zitafichwa kwa kufukiwa ardhini na kiasi cha sentimita 2 kutokeza kutoka usawa wa ardhi, zinaweza kutafutwa kwa njia kigundua chuma. Ikiwa saruji haipatikani, nondo za chuma pekee zinaweza kutumika, lakini njia hii inaweza kukabiliwa na wizi, na hatari ya kupata kutu.
- Vipande vya chuma vilivyotiwa uzio (urefu wa m 1.2) vinaweza kuwekwa kwa saruji kwa kina cha mita 0.5 kwa kutumia mashimo yaliyochimbuliwa kwa kutumia na kinu cha udongo.
- Alama za Feno ni chaguo ghali zaidi lakini linaloweza kudumu kwa muda mrefu
- GPS zenye usahihi wa kiwango cha juu zinaweza kutumika badala ya alama zingine za kudumu kama nguzo na saruji, lakini hii itawalazimisha watumiaji wengine wote baadaye kutumia vifaa vya gharama kubwa kama kama vilivyotumika wakati wa uwekaji wa kamba za kupimia kipenyo. GPS za kawaida hazina usahihi wa kutosha kugundua pembe za kamba za kupimia kipenyo, ni vizuri kutumia aina fulani fulani za alama halisi kwa ajili ya utambuzi wa pembe za kamba za kupimia kipenyo.

Kwa kila ploti mpya, orodha kamili ya data ya ploti (wakati fulani huitwa taarifa kuhusu data, lakini kimsingi ni maelezo kuhusu ploti) inapaswa kurekodiwa (ona Kiambatisho 1). Taarifa hii ni ya haraka kurekodi (mengi yanahitaji jibu la Ndiyo/Hapana) na itaruhusu data za ploti kutumika kwa aina mbalimbali za uchanganuzi. Data hii imegawanywa katika sampuli na data ya uharibifu, ambayo ina karatasi tofauti za data zinazopatikana kwenye tovuti ya SEOSAW.
Sampuli za data ya kurekodi inajumuisha maelezo ya:

- Muundo wa ploti – ukubwa, umbo, na kiini halisi cha sampuli.
- Eneo la ploti – longitudo, latitudo ya kila kona/kituo. Hii inapaswa kurekodiwa na GPS iliyowekwa kwa wastani wa eneo la GPS kwa takribani zaidi ya dakika ~30, na inapowezekana inapaswa kurudiwa kwa siku nyingi tofauti ili kuboresha usahihi.
- Urefu, mteremko, mwelekeo
- Sampuli inafanywa ndani ya ploti – kundi lililopimwa na sampuli nyingine au vipimo vilivyofanywa
- Hali ya mazingira - mvua, tabaka la uoto, sehem ya ploti katika mwinuko, na uwepo wa vichuguu vya mchwa
- Data ya uharibifu wa msitu itajumuisha maelezo ya:
- Matumizi ya ardhi - hali ya kisheria, haki za mtumiaji, kutokea kwa uvunaji, na kilimo
- Moto - makadirio ya muda wa kurudi kwa moto na/au muda tangu kuungua mara ya mwisho, udhibiti wa moto, n.k.
- Majanga ya asili – vimbunga, ukame, mafuriko, n.k.
- Uwepo wa wanyama wakubwa wanaokula mimea - Tembo, Wanyama wanaoliwa, Wanyama Wasioua, Mifugo n.k.

4. MASHINA YA MITI

4.1 Nini cha kupima

Weka alama, pima na fanya utambuzi wa mashina yote ya miti (pamoja na mitambaa, mitende na mibuyu) kama:
a. Zaidi ya 50% ya msingi wa shina yapo ndani ya ploti; na

a. b. Mashina hayo yana kipenyo ≥ hadi kizingiti cha chini kabisa cha kipenyo kilichobainishwa katika hatua ifaayo ya kipimo (ikiwa ni pamoja na mashina yaliyokufa na yaliyoanguka, ambayo mwanzo wa shina lake hadi sehemu ifaayo ya kipimo linapakana liko ndani ya ploti)

b. Kiwango cha chini cha kipenyo kitaamuliwa na malengo ya utafiti, na muundo wa mimea kwenye eneo husika. Kipenyo cha shina lazima kiwe sm ≥ 5 au sm ≥ 10, hivi ni vizingiti vilivyozoeleka zaidi. Ikiwa nia ni kurekodi uandikishaji (yaani idadi ya miti nyongeza mzingo) ambayo imefikia kiwango cha chini cha kipenyo k.m. sm 5), inashauriwa kupima mashina yote kwa kipenyo kidogo kuliko hiki (k.m. sm 4 au sm 9). Hii itasaidia kuhakikisha kwamba makosa yaliyofanywa katika kuamua kipenyo hayaathiri makadirio ya kima cha miti nyongeza mzigo.

Itifaki hii inajumuisha vipengeleo mbalimbali kwenye upimaji wa nguzo, machipukizi na uotaupya (yenye shina ndogo kuliko kizingiti cha kipenyo cha chini) katika sampuli ndogo za ploti kuu (mashina ya miti midogo).

Ploti mpya zilizoanzishwa katika mtandao wa SEOSAW zinapaswa kuchagua kizingiti cha chini cha kipenyo kwa ploti kuu ya ama sm 10, sm 5, au sm 3 kulingana na malengo ya utafiti na mpangilio katika muundo kiungamiti. Kiwango cha chini cha kipenyo kilichochaguliwa kinapaswa kuhakikisha kuwa angalau mashina 200 yanapimwa ndani ya plotia (bila kuhesabu vipimo vilivyofanywa katika viwanja vidogo vidogo).

4.2 Kipimo cha kipenyo

4.2.1 Sehemu ya Kupimia Kipenyo

Ili kuwezesha vipimo vya marudio katika urefu na mwelekeo ule ule wa awali kwenye shina la mti husika, kipenyo kinapaswa kupimwa katika hatua iliyoainishwa ya kipimo (POM). Ploti zote katika mtandao wa SEOSAW zimepitisha utumiaji wa mita 1.3 au 0.3 m kama sehemu maalum ya kuchukulia kipimo cha kipenyp (POM). Ijulikane pia kuwa sehemu hii ya kuchukulia kipenyo (POM) sio lazima uwe urefu wa wima, lakini ni urefu wa mstari wa moja kwa moja shina kutoka ardhini hadi kwenye POM, hata ikiwa shina imeinama au imepinda.

Chaguo-msingi la mita 1.3 (POM) linapaswa kutumika isipokuwa endapo mashina mengi kwenye ploti hayafikii urefu wa mita 1.3, hapo chaguo-msingi la mita 0.3 (POM) linaweza kutumika.

Ikiwa POM chaguo-msingi la mita 0.3 linatumiwa, sampuli ndogo ya miti inapaswa kupimwa kwa mita 1.3 na 0.3 ili kuwezesha matumizi ya kipengele cha ubadilishaji kwa kulinganisha na ploti zilivyopimwa kutumia chaguo-msingi la mita 1.3 (POM) kama sehem ya kupimia kipenyo

Kijiti chenye alama kwenye urefu wa mita 1.3 au mita 0.3 kinaweza kutumika kutafuta POM chaguo-msingi kinaposimikwa aridhini sambamba na shina la mti. Mpima azingatie mambo yafuatazo:

- Miti yenye mashina pacha – Miti iliyotoa tawi/matawi chini ya POM chaguo-msingi (mita 1.3) inajumuishwa tu ikiwa shina yaliyo juu yanazidi kizingiti cha kipenyo kwenye POM changuo- msingi.Matawi haya nayaweza pimwa kama miti inayojitegemea
- Miti inayochipuka – Shina lililochipuka hupimwa tu ikiwa linazidi kipenyo cha chini zaidi kwenye POM ifaayo.
- Miti yenye mingongomti – Miti ambayo inamigongomti kwa urefu wake wote inapaswa kupimwa kwa POM chaguo-msingi.
- Kipimo cha POM kinapaswa kufanywa kwa upande maalum wa mti. Ubaguzi unapaswa kufanywa tu katika hali zifuatazo:
- Miteremko - Ikiwa shina liko kwenye mteremko, urefu wa POM unapaswa kupimwa kwenye upande wa kuteremka wa mti.
- Miti inayoinama - Ikiwa shina limeegemea upande wa mteremko, basi urefu wa POM unapaswa kupimwa kando ya ukingo ulio karibu zaidi na ardhi.

Kwa kawaida, kipenyo kinapaswa kupimwa kwenye POM chaguo-msingi isipokuwa inapotokea kuwa sehem hiyo haitoi uwakilishi mzuri wa kipenyo cha shina kwa mojawapo ya sababu zifuatazo:

- **Ulemavu -** Shina linapokuwa limeambatana na matatitzo kwenye eneo la POM chaguo-msingi, kwa mfano kwa sababu ya jeraha, uvimbe, upotevu wa gome, au tawi zinapaswa kusogezwa hadi sehemu ya sentimita 30 juu ya ulemavu.
- **Mashina pacha au yeney matwai -** Miti inayogawanyika kwa njia ya kawaida kwenye eneo la POM inapaswa kupimwa katika sehemu ya sentimita 30 chini ya uvimbe sehemu ya chini tawi lilipo.
- **Mgongomti na na mizizi ning'inizi** - Miti ambayo imeimarishwa au iliyo na mizizi iliyosimama kwenye POM chaguo-msingi inapaswa kupimwa sm 30 juu ya sehemu ya juu ya kitako au mzizi wa juu zaidi wa nguzo.
- **Mitambaa** – Mimea aina ya mitambaa imejumuishwa katika utafiti ikiwa ina kipenyo kikubwa zaidi ya kipenyo cha chini cha kipenyo katika hatua yoyote ndani ya mita 2.5 kutoka ardhini. Mitambaa inayotimiza kigezo hiki inapaswa kupimwa katika maeneo matatu, 3; i) katika mita 1.3 m sambmba na shina kutoka shina linapoanzia, ii) katika mita 1.3 iliyopimwa kwa wima juu ya ardhi; iii) kwa kipenyo kikubwa zaidi ndani ya m 2.5 ya ardhi, ikijumuisha ulemavu wowote. Njia hizi tatu huruhusu kulinganisha na itifaki zingine.

Ikiwa POM iliyorekebishwa haitoi uwakilishi mzuri wa kipenyo cha shina, basi POM inapaswa kusogezwa juu zaidi hadi uwakilishi mzuri upatikane. Ambapo POM nzuri haiwezekani au haiwezekani kwa sababu ya uharibifu wa shina zima, mbinu za nusu ya kipenyo zinapaswa kutumika (tazama sehemu ya 4.2.2).

Kwa mashina yote, urefu wa POM lazima urekodiwe. POM inaweza kupakwa rangi ili kuwezesha upimaji upya , ingawa rangi zenye asili ya mafuta zinaweza kusababisha kutokea kwa uvimbe kwenye gamba la mti zinapaswa kuepukwa. Vile vile ubandukaji wa magome ya miti, na moto vinaweza kuharibu alama za rangi baada ya miaka michache (ona sehemu ya 4.3.1). Lebo pia zinaweza kutumika kusaidia kuhamisha POM. Lebo zinapaswa kuwekwa sentimita 20 juu ya POM, ili ktahisihsa upimaji wa awamu ya pili na kusaidia kuongeza kasi ya upimji na kuepuka lebo kuathiri kipenyo.

4.2.2 Kupima kipenyo

Kipenyo cha mti kwenye POM chaguo-msingi au zile zilizorekebishwa lazima zirekodiwe kwa mashina yote. Ploti zitumike kupima mashina yenye kipenyo cha sm ≥ 5cm mashina madogo yanapaswa kupimwa kwa kipimo cha kalipa. Kipenyo kinapaswa kupimwa hadi mm 1 iliyo karibu zaidi, na kurekodiwa kwa sentimita na mahali pa desimali 1, hata ikiwa hii ni sifuri, k.m. 17.0 cm, sio 17 cm.

Miti mikubwa (Mara 10 zaidi ya kizingiti cha chini zaidi) ni muhimu sana kwa makadirio ya biomasi, na vipengele vingi vya ikolojia. Ili kutoa fursa ya kufanya ukahiki maradufu wa kuwepo kwa miti mikubwa, na kuepuka makosa yanayosababishwa na kukosa sehemu ya desimali, andika neno "*mti mkubwa*" katika maelezo ya mashina yote makubwa, > Mara kumi,10x ya kizingiti cha kipenyo k.m. sentimeta 50 DBH kwa ploti vyenye kizingiti cha 5 cm. Hii ni muhimu hasa.

Vipimo vya kipenyo vinapaswa kufanywa chini ya mitambaa midogo, epiphytes au mizizi kwenye shina (kwa kuinua mbali na shina na si kukata), na baada ya kusafisha POM ya gome huru na matakataka. Ikiwa mitambaa, epiphytes na mizizi haziwezi kuinuliwa mbali na shina ili kuruhusu mkanda wa kupimia kipenyo kupitishwa chini yake, mbinu za nusu kipenyo zinapaswa kutumika.

Njia za nusu kipenyo
Njia za nusu ya kipenyo zitumike pale ambapo haiwezekani kupima pande zote za shina k.m. ikiwa imeanguka na kulala chini, au ikiwa kuna mitambaa au mizizi ambayo haiwezi kuinuliwa kutoka kwenye shina, au ulemavu ambao hauwezi kuepukwa. Kipenyo cha shina kinaweza kukadiriwa kwa kupima kwa kalipa au kutumia mkanda wa kipenyo kwenye nusu tu ya mduara wa shina na kuzidisha thamani kwa mbili. Mbinu hizi zikitumiwa ifahamike katika fomu ya ukusanyaji wa data.

4.3 Kuweka alama na kuchora mashina

4.3.1 Kuashiria mashina

Lebo za kimetali zinaweza kutumika kuashiria utambulisho wa mashina kupitia nambari zao za upekee kwa kila hina. Iwapo vitambulisho vya metali vitatumika, basi zinapaswa kuning'inia kwenye shina la mti ili kwamba msumari uwe sm 20 juu ya POM ili kusaidia kuilenga sehemu ya POM kwa usahihi mti unapopimwa tena, na kuzuia uvimbe wowote unaosababishwa na msumari usiathiri vipimo vya kipenyo. . Ikiwa kuweka alama kwenye miti kunatarajiwa kuathiri jinsi ploti hizo zinavyotumiwa na watu au wanyamapori, njia mbadala ya kupachika vitambulisho kwenye miti ni kuzika tagi chini ya mti, chini kidogo ya uso wa ardhi.
"iliyotoweka" au kuthibitisha lebo ambazo hazipo wakati wa vipimo. Ili kuwa sawa, kona ya kusini-magharibi ya ploti ya mraba au mstatili inapaswa kutumika kama kianzio cha majira ya nutka 0,0.

Njia rahisi zaidi ni kutumia kamba ili kuizungusha ploti iliyo hapa chini na kukadiria umbali wa x kutoka umbali kati ya mistari hoyo miwili, na y kama inavyosomeka kwenye kamba ya kupimia. Jambo la kuangalia hapa ni kwamba unaweza kupoteza kwa urahisi uwezekano wa kufuatilia ni kama ipi uliyokuwa unafanyia kazi.

Kuashiria miti na vitambulisho vya chuma

Lebo ndogo ndogo kimetali ka ajili ya utambulisho wa miti zinaweza kununuliwa au kutengenezwa kwa mabati ya kuezekea (takriban sm 5 x 5) na kuorodheshwa kwa muhuri wa moto(muhuri wa indent chanya). Mabati ya paa yanapaswa kuwa karibu 0.6mm kwa unene. Lebo ambazo ni nyembamba sana huweza kuharibika haraka na zinahitaji kubadilishwa mara kwa mara; lebo ambazo ni nene sana ni vigumu kugonga na namba na hivyo kufanya nambe zisisomeke vizuri. Vitambulisho vilivyotengenezwa kwa nyenzo zisizoakisi au vikiwa vimepakwa rangi havina usimbufu mkubwa kwa wanyama kama Tembo ambao hawapendi kuona vitu vya kung'aa saana. Vitambulisho vinapaswa kushikamana kwa usalama kwa shina kwa kutumia msumari. Ni bora kutumia misumari ya alumini ya karibu 5 cm kwa urefu. Misumari ya aluminium haisababishi athari sana kwenye mti kwani haina kutu, japokuwa kazi ya kugolelea misumari kwenye miti migumu inawza kwa na changamoto kidogo, hivyo misimari ya chuma inaweza kuhitajika kutumika wakati fulani. Misumari inapaswa kupigwa kwa pembe ya chini kidogo ili iweze kupenya gome na iwe salama, lakini iwe na angalau sm 2 ili kuruhusu nafasi kwa mti kukua. Ikiwa kamba za kupimia kipenyo zimegawanywa katika vipande vinavyoweka alama kwenye mashina yote katika kila ukanda kwenye pande zinazopishana za shina inaweza kusaidia kutambua kila ukanda na kuweka vipimo vya shina katika mfuatano.

4.3.2 Uramanishaji wa mashina ya miti

Kwenye ploti za mraba, sehemu ya kila shina la mti inarekodiwa kwa kutumia majira ya nukta XY kutoka kona ya kusini magharibi/SW mwa ploti . Ijapokuwa hii ni chaguo la mtafiti, lakini ni muhimu sana. Viwianishi vya X-Y hupunguza makosa wakati wa kufuatilia mashina



4.3.3 Mashina yaliyokatwa, yaliyovunjika na kuanguka

Kwa kila shina kumbuka ikiwa:

• Kwa miti iliyokatika, iliyovunja na kuanguka - rekodic, na unaweza (japo ni hiari) kuweka asilimia ya makadirio ya shina iliyobaki kwenye ktako cha shina. Shina lililovunjika laweza kujatwa kuwa ni pale ambapo mti umevunjia lakini sehemu ya juu ya shina juu ya bado imeunganishwa, wakati "Kukakwa" au mgawanyiko au mwachano unaweza tajwa kuwa ni pale ambapo sehemu ya juu ya shina haina muunganisho tena na kitako cha shina la miti husika.

• Mti uliojeruhika – hapa vipimo vya aina mbili vyaweza kutumika:

- Asilimia ya kambi iliyoachwa wazi kutokana na jerahaa, i.e. gome halipo. Hii inapaswa kukadiriwa kwa pande 4 za shina, kutoka ardhini hadi urefu wa mita 2. Ikiwa imejeruhiwa, saizi ya jeraha inapaswa kurekodiwa kwa upana mkubwa na urefu wa sentimita.
- Kuwepo/kutokuwepo kwa kuvu kwenye gogo kunapaswa kurekodiwa kama kiashiria cha kuoza.
- Imeanguka – hii inamanisha mti ambao hauwezi kustahimili uzito wake wenyewe, NB Ikiwa shina halina mizizi kwenye udongo, halijumuishwi kwenye orodha ya shina, lakini badala yake litarekodiwa kama mabaki ya magogo/miti iliyokufa.
- Umeanguka - hufafanuliwa kama kutokuwa tena na uzito wake

4.4 Sifa nyingine za mashina hai

Sifa zifuatazo zinapaswa pia kuzingatiwa kwa kutumia majibu rahisi ya Ndio/Hapana (Y/N)

•Idadi ya miti nyongezamzigo tokea sensa iliyopita (yaani, sasa imeongezeka hadi kufikia kipenyo cha juu)

• Iko kwenye kichuguu cha mchwa

• Uwepo wa mitambaa kwenye mataji ya miti

• Kuwepo kwa kinyoosho kwenye mashina ya miti

• Kisiki; ikiwa shina limekatwa au kuvunjwa chini kuliko POM, basi inaitwa kisiki.

4.5 Uharibifu na vifo kwenye mashina ya miti

Kujua ikiwa shina la mti limekufa ni jambo gumu kwenye uoto wa savana. Ni vigumu kugungua ikiwa shina limekufa kweli, na wakati mwingine "bado lina dalili za uhai ndani yake". Kwa hivyo, ni muhimu kurekodi hali halisi ya shina likiwa hai au limekufa kwa angalau sensa moja zaidi baada ya tamko la awali la kifo. Hapa, tunaepuka kukiri kuwa shina limekufa, ispokuwa tumehakikisha kinagaubaga kuwa limekufa kabisa, tukirejelea mashina kama "machipukizi" ikiwa yanaonekana kufa. Unapaswa kutambua hali ya shina, hali na uharibifu wowote kwa kutumia misimbo iliyoko katika Jedwali 2.

4.5.1 Mashina yanazochipuka

Shina linapaswa kurekodiwa kama linalochipukia ikiwa tu, hakuna dalili ya utomvu chini ya gome kwenye POM chaguo-msingi, hakuna dalili za uhai kwenye taji lake eneo la juu ya POM, na iwapo lina dalili za uhai chini ya POM tu. Kwa mfano, machipukizi mapya yanatokea kwenye kitako cha shina.

Jedwali la 2: Maelezo ya hali ya shina, hali ya shina, na sababu ya uharibifu

Hali ya shina	**Modi ya shina**	**Chanzo cha uharibifu***
A = shina lenye uhai R = shina limekufa, lakini lina dalili za uhai mahali pengine (kwenye kitako au mashina zingine) D = shina limekufa, na mmea mzima umekufa	B = Umevunjika/umekukatwa (shina limetenganishwa na kitako) C = Mti umepanda mimea juu F = Umeanguka (haijitegemei wenyewe) G = Mashimo J = Umepoteza gome K = Kuvu, L = Umeegama (zaidi ya 15° kutoka kwa wima) M = uko kwenye mchwa N = Kuajiri mpya, P = Umevunjika (ila bado imesikamana na shina) Q = Haijulikani S = Umesimama T = Stump ya mti U = Umeng'olewa V = Umetoweka W = Liana, Y = Umejeruhiwa, Z = Mgonjwa	A = Baridi (sio tembo, sio wadudu) E = Tembo F = Moto H = Binadamu (umekatwa au Umeambuliwa) I = Baridi L = Radi M = Mchwa N = Mti jirani O = Nyingine (elezea kwa maelezo) Q = Haijulikani W = Upepo

* Kumbuka, kwa kawaida haitawezekana kubainisha sababu ya kifo kwa uhakika wowote na inapokuwa sababu ya kifo si dhahiri, basi, msimbo wa "Q - Haijulikani" unapaswa kutumiwa. Wakati sababu ya kifo ikiwa ni “binadamu”, ongeza maelezo yake yanayoonyesha mbinu k.m. kuambua, msumeno mnyororo, panga.

4.6 Utambuzi wa aina miti

Kila mti uliopimwa unapaswa kupewa jina la spishi au jina litokanalo na mohospishi[1] za spishi husika. Mtaalamu wa mimea aliye na ujuzi anapaswa kuwepo wakati wa kuanzisha ploti kwa ajili ya kutambua spishi kwa kutumia jina la kisayansi na/au jina la kienyeji linalotumiwa na wakazi wa eneo hilo. Ikiwezekana, vielelezo vya vocha za spishi zote na spishi zilizopo ndani ya ploti zinapaswa kukusanywa na kuhifadhiwa katika herbaria ya taasisi husika, au hebaria ya Taifa ama kutumwa kweney hebaria za kimataifa. Vielelezo vya vocha vinaweza kutumiwa

kuthibitisha majina ya spishi na kuweka majina ya kisayansi kwa sifa za maumbile ya mti. Vitambulisho hivyo aina za spishi vinaweza kuhakikiwa na kuboreshwa kadiri ploti upya zinapoendelea kupimwa.

[1]Mofospishi ni sifa za kimaumbile ya mti zinazotambulika na zinazoweza kutofautishwa kati ya mti na mti ambao jina lake la kisayansi halijulikani. Haya yanaweza kuwa 'majina ya spishi za kienyeji'. Vinginevyo, hata wakati watafiti wenye ujuzi wa mimea wanahusika katika kusimika ploti, mara nyingi kuna miti ya baadhi ambayo haiwezi kutambuliwa (k.m. kutokana na ukosefu wa vipengele muhimu vya uchunguzi vilivyopo katika matunda au maua). Katika hali hizi, ni muhimu kubainisha ni miti gani kote kwenye ploti inaonekana kuwa ya aina moja, hata kama jina la kisayansi haliwezi kuwekwa juu yake (k.m. kwa madhumuni ya kukokotoa uanuwai wa alpha).

Ukusanyaji na utayarishaji wa vielelezo vya vocha

